

HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE. ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (MB) ALIYOITOA WAKATI WA UWEKAJI WA MAWE YA MSINGI KATIKA UJENZI WA KITUO CHA POLISI CHA LAELA NA UFUNGUZI WA KITUO KIDOGO CHA TUNGO TAREHE 17 JANUARI, 2015.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Rukwa Ndugu Jacob Mwaruanda,
Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama (M),
Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,
(Mwakilishi) wa Mtendaji Mkuu wa MCA-T,
Kaimu Katibu Tawala Mkoa,
Meneja wa TANROADS Mkoa,
Makatibu Tawala Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo,
Wawakilishi wa wadau wetu waliotusaidia ujenzi wa kituo hiki,
Meneja wa Mradi wa Barabara kwa kiwango cha lami Laela -
Sumbawanga,
Viongozi wa Chama Tawala (CCM) na Viongozi wa vyama Vingine,
Viongozi wa Taasisi za Umma na Taasisi binafsi,
Viongozi na Watendaji wa Serikali,
Waandishi wa Habari.

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuuona mwaka mpya wa 2015 tukiwa salama. Pia Namshukuru Mungu kwa kuanza mwaka mpya wa kikazi kwa shughuli hizi zinazotukutanisha mahali hapa siku hii ya leo.

Napenda pia kuchukua fursa hii, kutoa salamu zangu za Heri ya Mwaka Mpya 2015 kwa Wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa kupitia hadhara hii. Ni wazi kuwa Mwenyezi Mungu katuvusha Mwaka 2014 kwa makusudi maalumu na si kwa bahati mbaya ili kila mmoja wetu aweze kushiriki kikamilifu katika kuuletea Mkoa wetu Maendeleo.

Wapendwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa,

Mtakubaliana na mimi leo kuwa katika ahadi alizozitoa Mheshimiwa Prof. Jakaya Mrisho Kikwete -Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkoa wa Rukwa asilimia 95 amezitekeleza. Hivi karibuni kumejitokeza maswali kutoka kwa wadau mbalimbali wengine wakisema kwamba hajatekeleza, wengine wakisema ahadi zilikuwa hewa, lakini nadhani ni kutokana na kukosa taarifa hasa kwa sisi watendaji tulioko huku. Nina furaha kuwafahamisha kuwa Mkoa wetu umeandaa rasmi taarifa ya utekelezaji ya ahadi za Mheshimiwa Rais na hata zile ambazo hakuahidi lakini kwa kuzingatia shida za watu na malalamiko mbalimbali yametekelezwa kwa kipindi hiki cha miaka 10 toka awepo madarakani. Taarifa hiyo iko katika hatua za kuchapisha vitabu na hivyo wengi wataweza kuzipata.

Leo kupitia hafla hii napenda kujikita katika eneo moja tu linalohusiana na usalama katika Mkoa wetu ambao uko mpakani na nchi jirani za Zambia, Congo na Burundi, na Mikoa ya jirani ya Mbeya na Katavi.

Katika ahadi ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni pamoja na kuimarisha hali ya ulinzi na usalama katika Mikoa ya mipakani. Katika kufikia malengo hayo, suala la uimarishaji wa miundo mbinu ikiwemo barabara lilikuwa ni jambo muhimu. Wote tumeshuhudia sasa ujenzi wa barabara kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga kwa kiwango cha lami umewezekana. Hali kadhalika jitihada zinaendelea kufikisha barabara ya lami toka Sumbawanga hadi Kasanga na Sumbawanga, Namanyere, Kizi hadi Kibaoni Mkoani Katavi. Maendeleo ya ujenzi wa barabara hizo ni mazuri.

Jambo la pili ni kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi Askari wetu ikiwemo Ofisi na makazi yao. Katika kipindi hiki mmeshuhudia jitihada mbalimbali zilizofanyika katika kuongeza vituo vya Polisi jirani na wananchi hususan katika Kata, Tarafa na Wilaya, pia kuanzisha Wilaya mpya za Kipolisi. Matokeo ya jitihada hizo ni pamoja na matunda tunayoyaona leo hii ya kuweka jiwe la msingi katika Kituo cha Laela ambacho ujenzi wake kimsingi umekamilika isipokuwa bado kuweka vifaa muhimu pamoja na samani za Ofisi. Lakini pia uzinduzi wa Kituo cha mpakani Tunko - Mkutano.

Wapendwa wananchi,

Naomba nitoe kidogo chimbuko la vituo hivi ambavyo leo hii tuko kwa ajili yake. Kwa muda mrefu toka nilipofika Mkoa huu niliwiwa na ndoto ya kuona kuwa Mkoa wa Rukwa umekuwa salama. Kupitia Mpango wa **“Rukwa Salama”** nilioanzisha 2012 nimekuwa na ndoto ya kutokomeza uhalifu katika Mkoa wetu na kuifanya Rukwa kuondokana na mateso ya uhalifu na unyanyasaji wa aina yoyote ikiwemo imani za kishirikina. Mkoa

ulianzisha jitihada za kuongeza vitendea kazi kama magari na nyumba za askari kwa kuchangisha kwa wananchi, na wadau mbalimbali. Pia kumekuwa na jitihada ya kuongeza vituo vya Polisi jirani na wananchi, na kuongeza idadi ya askari katika vituo kulingana na mahitaji yake.

Jambo jingine ni kuwa nilipokuwa safarini nikitokea upande wa Mkoa wa Rukwa kuelekea Mbeya nikifika daraja hili la Mkutano, dereva wangu inabidi ashuke ashushe bendera ya Taifa kwenye gari kwani tunaingia Mkoa mwingine. Lakini nilikuwa nahuzunishwa na mambo mawili; la kwanza ni kuona kuwa ninakotoka kuko giza hakuna nyumba yoyote ile na kunaonekana kama kumepwaya kidogo ikilinganishwa na upande wa Mbeya. La pili baada ya kushusha au kupandisha bendera kutegemeana na upande ninakotoka nakuta wenzangu ambao wako kwenye gari wanashuka wanaingia porini wananiambia mama samahani kidogo tuchimbe dawa, sasa na mimi ni binadamu nikiona hali ile, na mimi natamani ningeshuka ili nikapumue kidogo, lakini ukijiuliza maswali mawili unaona itifaki hairuhusu. Hata hivyo sikuishia hapo nikafikiria hayo yanatokea kwangu tu na wale abiria je wanaotoka Mbeya au Sumbawanga wao wanachimba wapi dawa zao? Hali kadhalika nikatafakari zaidi nikaona huu ndio mtindo wenyewe kwa barabara zetu nyingi hazina maeneo ya watu kupumulia.

Kwa upande wa kibiashara nikafikiria hivi mtu akihitaji kununua mpunga unaozalishwa Rukwa bondeni lazima aende huko hatuwezi tukaweka mahali ambapo wanaweza kufanya biashara au minada?

Leo napenda kukiri maneno ya mama Jane Goodall katika kitabu chake cha "The reason for hope", kuwa unaweza ukawa na mawazo mazuri lakini usizifikie kwa kuwa huna watu wa kukubeba au kukusaidia. Kwa bahati nzuri mimi leo ninayo ya kujivunia, ninayo ya kushukuru, ninayo ya kulia kwa furaha, kuwa kuna Tai mkubwa ambaye alisikia kilio chetu wana Rukwa, Tai mkubwa sana aliyeweza kutubeba sisi ndege wadogo mbayuwayu, akaruka juu na akatupa ushindi wa kuwa juu kuliko wote kwa kufanikisha azma ya ndoto hizi zinazounga mkono ahadi za Mhe. Rais ya kuona Rukwa inakuwa salama, watu wanasafiri salama, wakiwa na ulinzi wa kutosha, na maeneo salama na tena ya kisasa ya kuwawezesha kujihifadhi wawapo safarini.

Tai huyo si mwingine ni MCA(T). Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Rukwa, na Jeshi la Polisi, na kwa niaba yangu mimi mwenyewe napenda kutoa shukrani za kipekee kwa uongozi wa MCA(T) chini ya Mkurugenzi wao Martin Mchomvu kwa kazi hii kubwa na nzuri sana ambayo ni ya aina yake na nadhani haijawahi kutokea katika Mikoa mingine.

Namshukuru pia mwakilishi wake aliyekuja hapa kwenye tukio leo Ndugu Paschal Assey ambaye ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa MCA(T), pamoja na timu yake, kwanza kwa kupitia na kuhakiki wazo, kuridhia na kutoa "Support" iliyohitajika.

Nawashukuru waliofanikisha jitihada hizi akiwemo Eng. Msofe ambaye kuna siku nilimrudisha akiwa safarini Mbeya ili mradi aje anisikilize,

TANROADS chini ya Eng. Florian Kabaka, pamoja na Mkandarasi aliyefanya kazi hii kwa kiwango bila kuchakachua na Wadau wote.

Nawashukuru Jeshi la Polisi hususan Kamanda wetu wa Mkoa Jacob Mwaruanda, pamoja na wote wanaomsaidia kwanza kwa kuona umuhimu wa kuanzisha rasmi Wilaya ya Kipolisi ya Laela.

Basi nami kwa heshima hii tuliyopewa na hawa wenzetu wa MCA(T) nimesema kituo cha Laela kiweze kufunguliwa na mtu mzito zaidi yangu. Nimeshaongea na Mhe. IGP amekubali kutusaidia kuweka mambo yote yaliyobaki ili kituo hiki kiwe cha kisasa na cha kiwango.

Wapendwa wananchi,

Kuwa na vituo vizuri ni jambo moja, lakini ulinzi kamili si Polisi peke yake, bali unaanzia na wewe na mimi. Sisi sote lazima tutambue wajibu wetu wa kuisaidia Polisi, na si kuwaona Polisi kama adui. Tujitahidi kuwa watu wema na kuwafichua wote ambao ni wahalifu kwa ajili ya kuifanya Rukwa kuwa salama na kuwa mahali pazuri pa kuishi. Leo nashukuru ndoto imeanza kutimia. Hata hivyo kama nilivyoagiza hapo nyuma, nasisitiza yafuatayo:-

1. Halmashauri kwa kushirikiana na serikali ya kata na kijiji kuandaampango mkakati wa uendelezaji wa mpaka wa Tunko/Mkutano ili kuwezesha shughuli za kiuchumi na maendeleo ya jamii ikizingatiwa kuwa eneo hili ni uso wa Mkoa wa Rukwa. Mpango huo uzingatie upatikanaji wa ajira kwa vijana, na ujenzi lazima uzingatie viwango.

2. Wananchi wa kijiji cha Tunko na Mkutano waendeleze mahusiano mazuri yaliyopo kwa faida ya Mikoa hii miwili yaani Rukwa na Mbeya na Taifa kwa ujumla.
3. Halmashauri isaidie kujenga nyumba mbili za askari katika eneo la Tunko
4. Kutenga eneo kwa ajili ya Magereza ya Wilaya Laela
5. Kutenga eneo kwa ajili ya Mahakama ya Wilaya Laela.
6. Nimepokea maombi kutoka uhamiaji nao watengewe eneo.

Hii itawezesha huduma hizo kuwa pamoja na kuondoa usumbufu wa upatikanaji wa haki kwa wakati.

Ndugu Wananchi,

Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana Jeshi la Polisi kwa mafanikio haya makubwa mliyoyapata, waswahili wanasema “mmelamba dume”. Msisitizo wangu kwenu ni juu ya utunzaji wa majengo haya. Mara nyingi watu tunapenda vitu vizuri, lakini baada ya kuvipata inakuwa ni vigumu kuvitunza. Ni vema kuweka utaratibu wa matunzo, hasa katika suala zima la usafi, na ukarabati mdogo mdogo kwani usipoziba ufa utajenga ukuta. Mimi binafsi nitakuwa jirani kufuatilia juu ya matumizi bora ya majengo haya.

Baada ya maneno haya sasa nipo tayari kuzindua kituo kidogo cha polisi kilichoko mpakani hapa Tunko na kuweka jiwe la msingi katika kituo cha Wilaya ya Kipolisi Laela.

**“POLISI OYEEE” “KIJIJI CHA TUNGO OYEEE” “AMANI NA
UTULIVU OYEEE” “ UTII WA SHERIA BILA SHURUTI OYEEE”.**

Asanteni kwa kunisikiliza.

Eng. Stella Martin Manyanya (Mb)

MKUU WA MKOA

RUKWA